

## LEARNING BY EAR

### **"If a tree falls... - Deforestation in Africa"**

#### **EPISODE SIX: "Living in Harmony!"**

**AUTHOR:** Romie Singh

**EDITORS:** Thomas Mösch, Jan-Philipp Scholz

**PROOFREADING:** Natalie Glanville-Wallis

#### **List of characters EPISODE SIX:**

**Narrator**

**SCENE 1** Chika (f, 18)

**SCENE 2** Talib (m, 20) Chika (f, 18) "Themba" (f, 30, representing an ordinary member of the Women's Group)

**SCENE 3** Akiki (f, 7) Isi (m, 18)

**SCENE 4** Mulogo (m, 22) Isi (m, 18)

**SCENE 5** Chief (m, 40) Mother (f, 36) Chika (f, 18) "Themba" (f, 30) Group of Women

**SCENE 6** Akiki (f, 7)

## **INTRO**

Karibu kwenye *Noa Bongo Jenga Maisha Yako* na katika kipindi cha sita cha mchezo wetu mpya kuhusu uharibifu wa misitu.

Kisa hiki kinaendelea kwenye mazingira ya vita vyta wenyewe kwa wenyewe na kinaonyesha jinsi uharibifu wa misitu- ukataji wa miti na maeneo ya nyasi- ulivyonatiza maisha ya vijiji na kusababisha mzozo kati ya jamii mbili za wakulima. Sasa jamii hizo mbili zinajikuta zikiwa pamoja kwenye kambi ya wakimbizi ya Dovani na zimeanza kutafuta ufumbuzi sawa kwa matatizo ya siku za usoni.

Katika kipindi cha leo, Isingoma na Akiki wametamauka kwa kuwakosa ndugu zao Kato na Sesi mionganini mwa watu waliowasili katika kambi ya Dovani. Akiki ana ndoto- Anadhani ni ishara, lakini inaweza kumuagulia aliko dada yake? Jiunge nasi wakati ambapo Chika anawapongeza kina mama kwa kujihusisha na mbinu mpya za ukulima.

## **Episode SIX: “Living in Harmony.”**

## **1.MUSIC UP**

### **Scene 1**

**2.CHIKA NARRATOR:** Kambi ya Dovani inapendeza. Mimi na Talib tumekuwa tukilifanyia kazi shirika la *Saidia Afrika*. Ni shirika ambalo lilianzisha kambi hii kuwaweka wakimbizi waliokuwa wakikimbia vita vilivyozuka miezi sita iliyopita. Wanaume wamekuwa wakitengeneza nyua; kundi la vijana limekuwa likitayarisha mabango ya kutahadharisha umma kuhusu maji yaliyochafuka; kundi la kina mama limekuwa likihusika na kilimo kinachoandamana na upandaji miti – ni njia ya kuhifadhi miti na wakati huo huo kupanda mazao ya chakula kwenye eneo moja. Asubuhi hii tuliwasimamia kina mama waliokuwa wakipanda maharagwe aina ya soya!

## **Scene 2**

### **3.SFX morning ambience outside / women's voices**

- 4.MOTHER:** Maharagwe ya soya ni mazuri sana. Yanatupatia pia mafuta mazuri sana ya kupikia.
- 5.TALIB:** Naam, na yana madini yanayofaa mwilini.
- 6.CHIKA:** Tunaendelea vyema. Katika mtindo huu wa kupanda tunapaswa kupanda mazao baina ya miti.
- 7.MOTHER:** Na maharagwe ya soya yanamea vizuri sana katika hali ya hewa ya huku. Yamkini tutapata mavuno ya ziada tutakayotumia na mengi ya kuuza.
- 8.CHIKA:** Hilo ndilo lengo letu. Kumbuka mama Kipko, tunataka kubadilisha mimea kutegemea majira, wakati hakuna jua jingi tutapanda ngano badala ya maharagwe ya soya.
- 9.MOTHER:** Lakini tungali na tatizo la kuni za kupikia.
- 10.TALIB:** Tumetenga eneo la msitu kwa kuni. Lakini tutahitajika kila tunapoikata miti kuendelea kupanda miti mingine.
- 11.CHIKA:** Ndio sababu tumeanzisha kitalu cha miche, ili tuweze kupanda miti mipya. Lakini pia ni lazima tutafute njia za kutumia kuni chache.
- 12.MOTHER:** Tutajadiliana hayo leo alasiri.

**13.CHIKA:** Naam, kisha nitawaarifu wanachama jinsi ardhi hapa itakavyopendeza tukipanda mahindi, maharagwe na mimea ya dawa katika eneo moja na miti.

**14.MOTHER:** Ai Chika. Huenda wasikubali kurudi nyumbani kwao pindi ukiwaarifu hayo. Hata hivyo ninachelea labda majeshi yameteketeza misitu na mashamba kwa moto.

### **15.MUSIC UP**

### **Scene 3**

#### **16.SFX Daytime ambience outside. Cows/ birds.**

#### **17.SFX: SOUND OF DRAWING WITH CRAYONS ON PAPER**

- 18.AKIKI:** Ninapenda kuchora! Ona! ...huyu ni Kiroko.  
Kichwani mwake nimeweka alama ya mkasi kwa  
sababu anakunywa maji katika eneo letu.
- 19.ISI:** Vizuri. Mchoro wangu ni kumhusu msichana  
anayekunywa maji kwenye dimbwi lililotengewa  
ng'ombe. Nimemchora akafanana na Akiki!
- 20.AKIKI:** Mchoro mzuri sana Isi. Natamani ningejua  
kuchora hivyo. Nipe huo mchoro. Tafadhalil!
- 21.ISI:** Hapana. Mabango haya yanatakitakana  
kukamilishwa na kubandikwa upesi. Watoto  
wengi wanaendelea kuugua kwa kunywa maji  
machafu. Hata hivyo nitakuchorea mchoro wako  
maalum. Ninakuahidi.
- 22.AKIKI:** Asante.
- 23.ISI:** Je wajua ulikuwa ukiongea usingizini mwako jana  
usiku?
- 24.AKIKI:** Alaa! Nilisema nini?
- 25.ISI:** Ulizungumza kuhusu mti wa mbuyu na kujificha  
ndani.

**26.AKIKI:** Aaah ...ajabu...Ma amekuwa akinisimulia hadithi ya mzee aliyejificha ndani ya mti wa mbuyu.

**27.ISI:** Ni mtu gani huo?

**28.AKIKI:** Ni mti ambao unatumika kutengeneza aina fulani ya ngoma. Sifa zake ni nyingi.

**29.ISI:** Sawa. Naam, kuna wakati ulianza kuongea kwa sauti kisha ukataja jina la Sesi.

**30.AKIKI:** Kweli ? Sikumbuki lolote.

Oh oh! Huyo Mulogo anakuja. Nitakwenda kutafuta kuni na nitakwenda pamoja na Kirogo.  
Tutaonana baadaye Isi.

**31.FOOTSTEPS APPROACHING .**

## **Scene 4**

### **32.SFX Same ambience as Scene 3(Daytime ambience. Cows/birds.)**

**(Throughout the following scene Isi is always negative and depressed. Mulogo is energetic and brash!)**

**33.MULOGO:** aah ... Mtoto wa watu ananiogopa!

**34.ISI:** Nadhani kwa sababu ya kujifanya kwako.

**35.MULOGO:** Samahani! Hujapata habari za babako na ndugu zako?

**36.ISI:** Hapana. Pia hatujapata habari kuhusu jamaa za Akiki. Akh! Tusiyazungumze hayo. (**Big sigh**) Babako alituletea jiko fulani jana. Mamangu amekuwa akilitumia kupikia. Kazi nzuri hiyo!

**37.MULOGO:** Ati... jiko? Au ni kisa cha kwamba wazazi wetu hatimaye wameanza kuzungumza baada ya kununiana kwa miaka mungi?

**38.ISI: (soft laugh)** Yote mawili!

**39.MULOGO:** Na hilo jiko lina nini?

**40.ISI:** Babako ndiye aliyelitengeneza. Yeyote anaweza kuliunda kwa kutumia vyuma vikuukuu na udongo.

- 41.MULOGO:** Kazi yako hiyo. Kufurahishwa na ndoo tupu ya chuma iliyo na chemni ya udongo. Unaamini kweli vitu hivyo vistasuluuhisha chochote?
- 42.ISI:** Jiko hilo linatumia nusu ya kuni zinazotumiwa na jiko la kawaida. Hoja ni kuokoa miti tu!
- 43.MULOGO:** Basi kwa nini tutumie jiko ambalo bado litatumia kuni? Nikwambie kitu, Isi, kitu ambacho kitakuchangamsha?
- 44.ISI: (dry sarcasm)** Kwamba unataka kujenga kinu cha nishati ya nyuklia katika eneo la Abanto!
- 45.MULOGO: (upset)** Ajabu! Ikiwa hutaki kuzisikiza rai zangu nitakwenda zangu nikazungumze na mtu anayetaka kunisikiliza.
- 46.ISI:** Samahani.
- 47.MULOGO:** Mimi husema kila mara, si vizuri kupinga mambo kila wakati. Tabia hiyo haikupeleki popote Isi.
- 48.ISI:** Tazama, mimi mwenyewe hapa nilipo nina dhiki ajabu. Pengine babangu na ndugu zangu washafariki, unanipata?
- 49.MULOGO:** Haya. Sawa. Lakini maisha yanaendelea. Pole... Ama unataka niondoke?
- 50.ISI:** Hapana. Hapana. Sawa..
- 51.MULOGO:** Haya. Sikiza! Nina mawazo mapya mazuri. Ukitaka nitakuarifu.

- 52.ISI:** Naam. Niambie.
- 53.MULOGO:** Isi unaijua hiyo wanayoiita kwa kimombo  
“biogas”?
- 54.ISI:** Biogas? Ina nini?
- 55.MULOGO:** Nishati inayotokana na kinyesi.
- 56.ISI:** Ina nini?
- 57.MULOGO:** Inatoa nishati ya kupikia, kuwashia taa na pia ni  
njia ya kutupa taka. Sikiza... China na India kwa  
miaka mingi zinatumia nishati hii.
- 58.ISI:** Fafanua!
- 59.MULOGO:** Ndivyo ninavyofanya...unahitaji kinyesi cha  
binadamu wane na ng'ombe mmoja au wawili  
kwa mtambo unaohusika kukutolea nishati  
inayoitosha nyumba moja.
- 60.ISI:** Unatumia kinyesi cha ng'ombe na cha  
binadamu...? Aaakh yaak!
- 61.MULOGO:** Kinyesi cha ng'ombe na cha binadamu vina  
madini mengi pamoja na gesi. Mtambo  
unaohusika hutumia uchafu wote huo... vyakula  
vilivyooza... kila aina ya takataka..! Usiwe na  
wasiwasi, mtambo wenyewe huwekwa chini ya  
ardhi lakini unatoa nishati ya kutosha. Pia  
unaweza kutumia masazo ya takataka kama  
mbolea...ni mfumo unaofaa kwa mambo mengi.

- 62.ISI:** Ai! Unayajuaje yote haya?
- 63.MULOGO:** Mimi huenda kwenye maktaba iliyopo afisini.  
Kuna vitabu na majarida kuhusu nishati mbadala.  
Ukitaka nitakuonyesha.
- 64.ISI: (laughing softly)** Nilifikiri wewe huenda huko tu wakati Chika yuko!
- 65.MULOGO:** Hah! Unanielewa vibaya rafiki yangu. Chochote ninachoshika kukifanya, hukifanya kwa dhati ya moyo wangu. Uzuri wa mradi huu ni kwamba ni jambo la kudumu. Ndio mustakabali wetu— tayari aina hii ya mradi ipo.
- 66.ISI:** Hii ni hatua kubwa sana ya maendeleo ukilinganisha na watu wetu waliozoea kupikia kuni na kuchoma makaa.
- 67.MULOGO:** Si unasema unataka kuhifadhi miti? Basi zingatia mradi huu. Kweli... nakutanabahisha...huenda ukafikiri kwamba ninajititimua bure kumhusu Chika...ukweli wa mambo ni kwamba na yeye ninamzingatia kwa kina!

## **68.MUSIC UP**

## **Scene 5**

### **69. SFX Daytime ambience (under a tree) Voices of women**

**70.CHIEF APALOO: (Whispering)** Hujambo Bi Kipko. Je ni sawa nikikaa huku nyuma nisikilize? Ningependa kuyajua mawazo ya kina mama!

**71.MOTHER: (Whispering)** Sawa. Karibu. **(Louder)** Kina mama wenzangu. Ningependa kukifungua kikao. Natumai mtamkaribisha Chifu Apaloo ambaye anataka kushuhudia tunavyofanya! Amekuja kujifunza jinsi kina mama wanavyoandaa vikao kwa misingi ya kidemokrasia!

### **72.POLITE LAUGHTER**

**73.MOTHER:** Na sasa, leo mada kuu: mabango ya kutahadharishana kuhusu uchafuzi wa maji na njia mpya za kupunguza ukataji kuni. Chika?

**74.CHIKA:** Hapa tuna mabango kumi na matano. Mengi ya haya mabango yamechorwa na Isingoma na Akiki. Mnayaonaje?

### **75.SFX: POSTERS BEING SHOWN AROUND.....VOICES**

#### **APPROVING POSTERS**

**76.CHIKA:** Tafadhalini, waambieni watoto wenu watizame mabango na wanywe maji tu kutoka kwenye madimbwi yaliyotengewa binadamu. Ng'ombe wametengewa madimbwi yao.

**77.MOTHER:** Inatubidi sote kusoma mabango hayo! Haya basi!  
 Twende kwenye mada nyingine. Tungependa  
 kuzungumza kuhusu majiko yetu na shida ya  
 kutafuta kuni. Nani ana jambo la kusema?  
 Yeyote? Naam, Bi Themba?

**78.THEMBA:** Ninachukia kwenda kutafuta kuni. Ningependa  
 kupanda mimea kama tulivyofanya hivi leo  
 asubuhi.

**79.CHIKA:** Nakubaliana na Themba. Ndio njia bora ya  
 kutumia wakati na nguvu zetu. Hiyo kazi ya  
 kubebana na kuni kwa muda mrefu – mtu  
 anahitaji nusu ya siku. Tena kwa kupika kwa siku  
 moja.

**80.MOTHER:** Nawaona wasichana wadogo wakifanya hivyo. Ni  
 kupoteza wakati na vipaji vyao. Wanapaswa  
 kuwa masomoni.

**81.THEMBA:** Sote tunateseka. Na kuni zenyewe zinatoa moshi  
 mwingi. Sote tunakohoa na ni wagonjwa.

**82.MOTHER:** Naam. Nachukia kujikunyata kwenye mafiga  
 yangu matatu jikoni. Tunapaswa kuwa na majiko  
 mazuri ii tutumie wakati wetu mwingi kwa  
 shughuli za manufaa kama vile kilimo.

### **83.WOMEN APPROVE**

**84.CHIEF APALOO:** Samahani. Naomba mniruhusu kidogo. Nina  
 jambo nataka kusema.

**85.MOTHER:** Bila shaka. Endelea.

**86.CHIEF APALOO:** Nasikitika sana kusikia jinsi maisha yalivyo magumu kwenu kina mama. Zama za mamangu ilikuwa rahisi kupata kuni lakini sasa inawabidi kutembea kwenda mbali. Hali inazidi kuwa ngumu kila uchao. Asante sana Bi. Kipko kwa kunipa fursa ya kuwaonyesha jiko hili. Natumai kina mama mtakubali. Litawapunguzia usumbufu mlionao.

**87.MOTHER:** Asante Chifu Apaloo. Sasa...ningependa kuwaonyesha... jiko la kombora...

#### **88.VOICES OF SURPRISE AND LAUGHTER**

## **Scene 6**

### **89.SFX Distant voices. Cow noises/mooing**

### **90. LOW MUSIC UP SIGNALLING DANGER. HOLD UNDER (OPTIONAL!)**

**91.AKIKI:** Kiroko. Lazima uweke siri. Ninakwenda kuutafuta mbuyu. Nilikuwa na ndoto. Ninaamini dada yangu yuko kwenye mti huo. Inanibidi kuutafuta huo mti, kama yule mzee wa hadithi ya Mama Kipko. Mti wenyewe uko katika mwitu wa Abanto. Ninajua...pindi nikiupata huo mti nitampata Sesi wangu.

### **92.MUSIC UP**

## OUTRO.

Ni hayo tuliyokuandalia kwa leo katika kipindi cha *Noa Bongo Jenga Maisha Yako* kiitwacho “Mti unapoanguka...”, kilichoandikwa na Romie Singh, kinachoshughulikia suala la uharibifu wa misitu. Katika kipindi chetu kijacho, kina mama wanaanza kufaidika kwa jasho lao, na – kiwewe si kiwewe Akiki anapokimbilia kwenye maeneo ya vita kumtafuta dada yake mwituni. Usikose kujiunga nasi katika kipindi cha saba upate kujua mambo yatakavyokuwa. Kumbuka, ukitaka kusikiliza tena kipindi hiki au kuwaarifu marafiki zako kukihusu, tafadhali tazama wavuti wetu

[www.dw-world.de/lbe](http://www.dw-world.de/lbe)

Kwaheri kwa sasa!

**END OF EPISODE 6**